Ruvuma walivyodhamiria kuanzisha hifadhi ya wanyamapori kisiwani Lundo

Na Albano Midelo

MKUU wa Mkoa (RC) Ruvuma, ameagiza Mamlaka ya Kusimamia Wanyamapori Tanzania (TAWA) wapeleke wanyamapori kwenye Kisiwa cha Lundo ziwani Nyasa.

RC Christina Mndeme, akizungumza katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alagiza TAWA wapeleke wanyamapori kwenye kisiwa hicho kilichoko ziwani humo wilayani Nyasa.

RC Christina, baada ya kuagiza hivyo, alisistiza kwamba kupelekwa wanyamapori kwenye kisiwa hicho itasaidia kuongeza watalii, na kwamba **mawiana na** lengo la kutangaza vivutio vya kitalii vilivyoko Wilaya ya Nyasa, ambako kumetangazwa kuwa kitovu cha utalii mkoani Ruvuma.

Pia, RC Christina aliagiza wadau wa utalii na hifadhitengefu, ikiwemo TAWA na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), wachukue jukumu la kueneza ueiewa kuhusu uhifadhi na utalii, hasa kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, ili waiue jinsi sekta ya utalii inavyoweza kuwezesha kuchochea uchumi.

RC Christina vilevile aliagiza kwamba ushoroba na mapato yatokanayo na wanyamapori mkoani Ruvuma viteshimiwe na kulindwa, kwa sababu ni moja ya rasilimali za nchi. Adha, aliagiza kwamba wananchi wote waliovamia maeneo hayo waondolewe haraka.

Kufuatia maagizo hayo, wadau wa utalii mkoani humo, ikiwemo TAWA, TANAPA na Wakala ya Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wameanza kutekeleza hatua kadhaa, ikiwemo azma ya kuanzisha hifadhi ya kufuga wanyamapori kwenye Kisiwa cha Lundo, pamoja na kufuga ndege katika Kisiwa cha Mbambabay.

Mshauri wa Maliasili na Utalii Mkoa wa Ruvuma, Afrikanus Challe, anasema kuwa wanataraja kuanzisha hifadhi Mbambabay, ambayo itajumuisha visiwa vya Lundo na Mbambabay pamoja na milima ya Mbamba, Tumbi na Ndengere, vyote viko wilayani Nyasa.

Challe anasema kuwa, hifadhi ya Mbambabay itakuwa na ukubwa wa eneo la hekta 597, na kwamba maeneo hayo yanafaa kufugia wanyamapori na ndege.

Anasema kwamba, kati ya hekta hizo, Milima Mbamba wenye eneo la ukubwa hekta 40, Milima Tumbi hekta 110 na Kisiwa Mbambabay hekta 27, kutakuwa maalum kwa ufugaji ndege, wakati TAWA wanataraja kupeleka wanyamapori jamii ya swala kwenye Kisiwa cha Lundo chenye ukubwa wa hekta 20.

"Milima na visiwa hivi vimejaliwa kuwa na uoto mzuri wa miombo, mawe yanayozunguka visiwa hivi, na milima kandokando ya ziwa yanahifadhi samaki adimu wa mapambo zaidi ya aina 400," Mshauri wa Maliasili na Utalii Ruvuma huyo anasema.

Challe anasema kuwa, eneo la hifadhi ya Mbambabay ni muhimu sana kwa upande wa Tanzania, hususan kwa matumizi ya shughuli za utalii kama vile utalii wa kuvua samaki, kupiga mbizi, yatching, utalii wa kuendesha mitumbwi na kuweka kambi kwenye fukwe.

Anasema kuwa, eneo hilo likihifadhiwa litatumika kwa ajili ya mazalia ya samaki, na kwamba hiyo itaongeza vipato vya wananchi wanaotegemea shughuli za uvuvi.

"Mbambabay ikihifadhiwa inaweza kuleta ushindani kibiashara hapa nchini, kwa sababu katika nchi yetu hakuna eneo linaloweza kutoa mchanganyiko mzuri wa huduma za kitalii kama zitakazotolewa katika eneo hili," Challe anadokeza.

Uchunguzi uliofanyika Malawi umebaini kuwa, nchi hiyo ina hifadhi kadhaa za taifa kwenye Ziwa Nyasa.

Hifadhi hizo ni pamoja na Lake Malawi National Park na Cape Mcclear Nature Reserve ambazo huuza huduma za kitalii kwa kutumia rasilimali zilizomo ziwani humo.

Kisiwa cha Lundo kipo kwenye Ziwa Nyasa.

Milima ya Mbamba iko mjini Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma. (Picha zote na Mpigapicha Wetu)

Mshauri wa Maliasili na Utalii Mkoa wa Ruvuma anasema Idara ya Maliasili na Utalii Ruvuma wamekusudia kutekeleza azma ya serikali kwa vitendo, kwa kuharakisha mchakato wa kukuza biashara ya utalii na kuwezesha Mbambabay iwe kitovu cha utalii mkoani humo –

Afisamaliasili na utalii huyo mkoani humo anasema kuwa, kutokana na Malawi kupata mafanikio kwenye Ziwa Nyasa upande wa nchi hiyo, Mkoa wa Ruvuma nako inatakiwa wajongeze kwa ubunifu, ili nako waanze kutoa huduma ambazo ni tofauti, pamoja na zile zinazotolewa Malawi.

"Mamlaka ya wanyamapori Tanzania ifanye juhudi za kuutambua huduma zinazotolewa katika hifadhi za Malawi zilizopo ndani ya ziwa na pembezoni mwa Ziwa Nyasa," Challe amesihauri.

Afisamaliasili huyo anasema kuwa, maeneo yote yaliyopendekezwa kuongezwa katika mradi huo hayatumiwi katika shughuli za kibinadamu, isipokuwa maeneo machache ambayo yanatumiwa na wavuvi kwa kiasi kidogo, kwamba hivyo hataathiri hifadhi hiyo mpya.

Anasistiza kuwa, kutokana na uduogo wa visiwa vya Mbambabay na Lundo, inapendekezwa katika maeneo hayo kusijengwe makazi ya kudumu, na kwamba wafanyakazi wa kuhudumia watalii ni vema wawe na makazi nje ya kisiwa, ili kuendeloa kutunza uoto wa asili ulopo.

"Hii ni hifadhi ya pekee ya wanyamapori pamoja na samaki wa mapambo, itakuwa hifadhi ya Ziwa Nyasa ambayo itavutia watalii kutoka kusini.

"Hivyo kutekeleza sera ya nchi ya kufungua biashara ya utalii kusini," anasema.

Challe anasema kuwa, hifadhi hiyo itasidia kulinda mipaka ya Tanzania iliyopo kusini kwenye Ziwa Nyasa, na kwamba itatambulisha duniani jinsi Tanzania inavyomiliki sehemu ya Ziwa Nyasa, tofauti na nchi jirani ya Malawi inavyodai.

Amepongeza hatua ya Serikali ya Mkoa wa Ruvuma ya kuagiza milima ya Mbamba, Tumbi na visiwa vya Lundo na Mbambabay kukabidhiwa kwa TAWA, ambao hivi sasa ndiyo wakokabidhiwa dhamana ya kutunza hifadhi za wanyamapori, kwa niaba ya serikali na wananchi kwa ujumla.

Anasema kuwa, Idara ya Maliasili na Utalii Ruvuma wamekusudia kutekeleza azma ya serikali kwa vitendo, kwa kuharakisha mchakato wa kukuza biashara ya utalii na kuwezesha Mbambabay iwe kitovu cha utalii mkoani humo.

Hivi karibuni, wakati waziri mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Ruvuma, alitoa rai kwa Watanzania ndani na nje ya nchi kuwa wawekeze wilayani Nyasa ambako kuna vivutio vya kila aina, ikiwemo mundombinu bora ya barabara za lami, meli tatu kwenye Ziwa Nyasa pamoja na huduma za kijamii kama umeme ambazo zimeboreshwa.

Serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 129 kujenga barabara ya lami toka Mbinga hadi Mbambabay wilayani Nyasa ambayo ina urefu kilomeli

Pia, serikali itoa zaidi ya bilioni 20 kwa ajili ya ma kuhuduma usafirishaji Ziwa Nyasa.

Scanned with CamScanner